MKATABA KUPANGISHA GHALA

**MKATABA** umefanyika leo tarehe 27 mwezi 03 mwaka 2023

**KATI YA**

**ELIZABETH RICHARD MOSHI** wa S. L. P 51, MARANGU ambaye kwenye makubaliano haya atajulikana kama "**MMILIKI**" neno ambalo litajumuisha yeye, warithi wake na wote watakaodai haki kutokana na mkataba huu kwa upande mmoja

**NA**

**IZACK ENTERPRISES LIMITED** Kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya S. L. P 318, MOSHI Tanzania, ambayo kwenye Mkataba huu itajulikana kama "**MPANGAJI** "neno ambalo litajumuisha yeye, warithi wake na wote watakaodai haki kutokana na mkataba huu kwa upande mwingine.

KWA KUWA **ELIZABETH RICHARD MOSHI** ni mmiliki halali wa Ghala liliyopo **Plot No. 16, 17 & 18, Farm 181/182,** Manispaa ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro, hivyo kwa hiari yake mwenyewe anakubali kumpangishia **Mpangaji** Ghala hilo kwa muda wa miaka **mitatu** (3) kuanzia tarehe 01 mwezi **Septemba mwaka 2022** mpaka tarehe **30** mwezi **August** mwaka **2025** bila kubugudhiwa kwa kuzingatia makubaliano yaliyopo kwenye mkataba huu.

**HIVYO BASI, MKATABA** huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo:-

1.0 **Kwamba**, mmiliki amempangishia mpangaji ghala tajwa hapo juu lililopo Plot No. Plot No. 16, 17 na 18, Farm 181/182, Manispaa ya Moshi kwa malipo ya kodi ya **shilingi za kitanzania milioni thelathini na sita tu (Tshs. 36,000,000/=)** kwa muda wote wa miaka mitatu ambayo italipwa kwa awamu tatu.

   1.1 Kodi ya mwaka wa kwanza ilishalipwa jumla ya shilingi za kitanzania **milioni kumi na mbili tu (Tshs. 12,000,000/=)** mnamo tarehe 19/08/2022 kupitia mkataba uliosainiwa kati ya Elia Richard Moshi na Izack Enterprises Ltd

   1.2 Kodi ya mwaka wa pili italipwa jumla ya shilingi za kitanzania **milioni kumi na mbili tu (Tshs. 12,000,000/=)** mwishoni mwaka wa kwanza wa mkataba huu yaani tarehe 01/09/2023

   1.3 Kodi ya mwaka wa tatu italipwa jumla ya shilingi za kitanzania **milioni kumi na mbili tu (Tshs. 12,000,000/=)** italipwa mwishoni mwa mwaka wa pili wa mkataba huu yaani tarehe 01/09/2024.

2.0 **Kwamba**, ghala tajwa hapo juu litatumika kwa shughuli halali za kibiashara ikiwemo kuhifadhi bidhaa za *Izack Enterprises Limited* zinazoruhusiwa na sheria na taratibu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3.0 **Wajibu wa Mpangaji**



Scanned with CamScanner CamScanner

3.1 Kulipa Kodi ya pango ndani ya muda kama ilivyoainishwa hapo juu kwenye Mkataba huu

3.2 Mpangaji anatakiwa azingatie usafi wa ghala ndani na nje pamoja na mazingira yake na anatakiwa atumie ghala tajwa kwa matumizi yanayozingatia sheria na taratibu za nchi tu na si vinginevyo.

3.3 Mpangaji anatakiwa alipie gharama zote zitakazojitokeza katika upangaji wake mfano, maji, umeme, taka, kodi na malipo yeyote yatokanayo na uendeshaji wa ghala tajwa hapo juu kwa muda wote wa uhai wa mkataba huu na wakati wa kuondoka katika ghala tajwa atahakikisha kuwa hataacha deni lolote linalohusiana na matumizi ya ghala tajwa hapo juu.

3.4 Kwamba kodi zote za serikali zitokanazo na uendeshaji wa ghala tajwa hapo juu zitalipwa na mpangaji

**4.0 Wajibu wa Mmiliki**

4.1 Mmiliki, kwa wakati muafaka anayo haki ya kuingia katika ghala hilo pale inapobidi ili kukagua au kufanya ukarabati wa ghala hilo au kuchunguza endapo kuna dosari yoyote iliyojificha. Hivyo mpangaji atataarifiwa kuhusu hilo na kwamba ni vizuri iwe katika masaa ya kazi.

4.2 Kufanya ukarabati wa ghala pindi itakapohitajika

4.3 Kulipa kodi ya ardhi

4.4 Hatampangisha Mpangaji mwingine kwa kipindi chote cha Mkataba huu

**5.0** Kwamba, mpangaji haruhusiwi kumkodishia mtu mwingine ghala tajwa hapo juu bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa mmiliki, na ikiwa Mpangaji atashindwa kuendelea na Mkataba basi mpangaji atamrudishia ghala mmiliki na kukabidhiana kwa maandishi kama ilivyokua wakati wa kuingia.

**6.0** Kwamba jukumu la mmiliki ni kufanya matengenezo makubwa kwenye ghala tajwa hapo juu na endapo mpangaji atahitaji kufanya marekebisho yoyote makubwa atahitaji ruhusa ya maandishi kutoka kwa mmiliki wa ghala.

**7.0** Kwamba, ikitokea upande wowote kwenye mkataba huu ukavunja masharti ya mkataba huu upande wowote una haki ya kuvunja Mkataba huu bila kutoa notisi yoyote.

**8.0** Kwamba Mkataba huu utakapofika mwisho wake na kama mpangaji ana nia ya kuingia Mkataba mpya atahitajika kutoa taarifa ya maandishi mwezi mmoja kabla ya Mkataba huu kuisha na mmiliki atahitajika kujibu taarifa hii ndani ya mwezi mmoja kabla mkataba huu kufikia mwisho.

**9.0** Kwamba endapo kutakuwepo na sababu za msingi zitakazopelekea upande wowote kwenye mkataba huu kuvunja mkataba huu itabidi taarifa [notisi] ya



Scanned with CamScanner

maandishi ya nia ya kuvunja mkataba huu ya siku thelathini [30] itolewe. Endapo mmiliki wa ghala ndiye atakuwa ametoa notisi ya kuvunja mkataba huu atahitajika kurejesha kodi ya miezi iliyosalia katika mkataba huu na endapo ni mpangaji kiasi cha kodi kilicholipwa hakitarejeshwa.

**10.0** Kwamba, endapo kutatokea mgogoro wowote katika kutafsiri utekelezaji wa mkataba huu sheria zitakazotumika ni sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KWA USHUHUDA** na **UTHIBITISHO**, mkataba huu umewekwa saini na mmiliki na mpangaji leo tarehe 27 mwezi 03 mwaka 2023 kama inavyoonyeshwa hapa chini:

**IMEWEKWA SAINI** na **KUTOLEWA**
na **ELIZABETH RICHARD MOSHI**
ambaye ninamfahamu/ametambulishwa
kwangu na ______
leo tarehe 27 mwezi 03 2023

______ **MMILIKI**

**MBELE YANGU:-**
Jina: Emmanuel Pascal Karia
Anwani: 931, Moshi
Saini: ______
Wadhifa: **WAKILI & KAMISHNA WA VIAPO**

Emmanuel Pascal Karia
Box 931 Moshi
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

**IMEWEKWA MUHURI** na **KUTOLEWA**
na **IZACK ENTERPRISES LIMITED**
leo tarehe 27 mwezi 03 2023

______ **MPANGAJI**

1 Saini ______
Jina: CLARA L. MAKUNDI
Wadhifa DIRECTOR- IZACK ENTR. LTD.

2 Saini ______
Jina: MOHAMED JAMBALAGA
Wadhifa HR MANAGER- IZACK ENTR. LTD

**MBELE YANGU:-**
Jina: IBRAHIM A. KOMU
Anwani: 8992 Moshi
Saini: ______
Wadhifa: **WAKILI & KAMISHNA WA VIAPO**

IBRAHIM A. KOMU
ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS
P.O. BOX 8992 MOSHI



Scanned with CamScanner